**Learning by Ear 2011 – Road Safety**

**Episode 07 – Motorbike riders wear helmet and safety strip**

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck, Katrin Ogunsade**

**Proofreading: Martin Vogl**

## CHARACTERS:

Onyesho la 1:

- GRACE (UMRI WA MIAKA 70-80, mama yake Pamela)
- PETER (UMRI WA MIAKA 60-70, baba yake Samuel)

Onyesho la 2:

- GRACE (UMRI WA MIAKA 70-80)
- DEREVA 1 (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 18-25)
- DEREVA 2 (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 18-25)
- PETER (UMRI WA MIAKA 60-70)

Scene 3:

- GRACE (UMRI WA MIAKA 70-80)
- DEREVA 1 (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 18-25)
- DEREVA 2 (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 18-25)

Scene 4:

- GRACE (UMRI WA MIAKA 70-80)
- PETER (UMRI WA MIAKA 60-70)
- DEREVA 1 (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 18-25)

Intro/Studio/Outro:

- MTANGAZAJI BEATRICE (MWANAMKE)
- GEORGE – MTAALAMU WA USALAMA BARABARANI (MWANAMUME)

## Intro:

**1. Beatrice:** Karibu kwenye makala ya Noa Bongo Jenga Maisha yako na mchezo wetu wa redio kuhusu usalama barabarani. Jina langu ni Beatrice. Kwenye vipindi vyetu vyote kumi tunaandamana na familia ya Wanjiru. Tunaangazia maisha yao ambapo walishuhudia maafa yanayotokana na ukosefu wa usalama barabarani barani Afrika. Tunazungumza pia na mtaalamu wa usalama barabarani ili tujue jinsi ya kuhakikisha usalama zaidi barabarani kwa lengo la kuokoa maisha. Katika kipindi kilichopita, Grace, mama yake Pamela, anasafiri safari ndefu kwenda mjini. Lakini basi analosafiria linapata ajali kwa sababu ya dereva kusinzia akiwa kwenye usukani. Katika kipindi hiki inawabidi Grace na Peter kupelekwa nyumbani kwa pikipiki. Lakini Grace anashtuka kwa kuwa waendesha pikipiki hawavai kofia za usalama wala mavazi yanayong'aa kuhakikisha usalama barabarani.

## Scene One: At the bus station

**2. SFX Atmo: buses coming and going**

**3. GRACE:** Bado hakuna teksi, Peter. Tufanye nini sasa? Tutafika vipi nyumbani? Nimechoka.

**4. PETER:** Ninajua. Nadhani ni wakati wa watu kutoka kazini. Tusubiri kiasi dakika kumi zaidi. Vinginevyo itatubidi tutumie pikipiki.

**5. GRACE:** Na umri wangu huu wa takriban miaka themanini. Unataraji nipande pikipiki na umri wangu huu?

**6. PETER:** Hatuna jingine. Hatutakaa hapa kusubiri. Tukikosa teksi itatubidi tuagize pikipiki zile pale. La sivyo tutakaa hapa kwa muda mrefu.

**Scene Two: Getting on the motorbikes**

**7. SFX Atmo: buses coming and going in the distance**

**8. SFX: motorbike starting up**

**9. GRACE:** Dereva, kofia yangu ya usalama i wapi? Na wewe mbona huna kofia ya usalama?

**10. DRIVER 1:** Hatuna. Zina faida gani, kuna joto kweli kweli hapa mjini, nani anahitaji kofia ya usalama? Bora kuendesha huku nikiwapungia mkono madereva wengine barabarani kuliko kuwa na hiyo kofia. Tena nina hakika kwamba kofia yenyewe inamzuia mtu kuona vizuri anakoelekea.

**11. GRACE:** Una kichaa? Siwezi kupanda pikipiki bila kofia ya usalama mimi. Mji huu madereva wake twawajua walivyo kama wendawazimu na tena magari mengi ni makubwa kuliko pikipiki yako hiyo. Hiyo pikipiki ikagongwa tutanusurika?

**12. DRIVER 2:** Mama wacha wasiwasi. Kuna shida gani? Panda kwenye pikipiki twende. Wajua tuna kazi nyingi.

**13. PETER:** Fanya bidii Grace. Hatuna jengine la kufanya. Pikipiki tu ndiyo itakayotufaa. Waona jinsi magari yalivyo mengi barabarani nab ado teksi hazipo.

**14. GRACE:** Peter. Siwezi. Hata kama mwenyewe ataniahidi kwamba ataendesha pikipiki yake taratibu sipandi. Tayari nimeshaona jinsi magari, mabasi na malori yanavyozichukulia pikipiki.

**15. DRIVER 1:** Mama, kama huendi shuka nimbebe abiria mwingine, sawa? Unanipotezea wakati.

**16. PETER:** Grace, jimakinishe vizuri kwenye pipiki kwa kuwa si mwendo mrefu, pengine kiasi dakika 20. Kwa hisani yako. Pamela na watoto wanatusubiri nyumbani.

**17. GRACE:** **(with fear and doubt)** Mbona nimekuja mjini? Heri ningebaki nyumbani. Kwanza mambo ya basi kisha haya sasa. Sielewi kwani watoto hawa hawazingatii usalama. Tangu lini mwendesha pikipiki akakosa kofia ya usalama? Hatari sana…sipendi hata kidogo! Lakini bila teksi tufanye nini… **(pausing, convincing herself)** Sawa, nitapanda! Lakini huo ndio mwisho. Nitarudi zangu nyumbani kesho asubuhi na mapema.

**18. PETER:** Asante, Grace! **(to the driver)** Sawa, tunaweza kuondoka.

**19. SFX:** **motorbikes starting up and driving away**

**Scene Three: driving along on the motorbikes**

**20. SFX Atmo: driving along the streets, traffic, honking of horns**

**21. DRIVER 1:** **(shouting)** Tunakwenda mtaa gani?

**22. GRACE:** **(shouting back)** Nadhani ni baada ya majumba matatu kutoka hapa… Ebu muulize Peter kwenye ile pikipiki nyingine. Muda mrefu tangu nilipokuja huku mara ya mwisho kwa hivyo sikumbuki vizuri!

**23. DRIVER 1:** **(shouting to driver 2)** Aisee, muulize abiria wako wapi tunakokwenda!

**24. DRIVER 2:** **(shouting back)** Wewe tufuate tu, sasa hivi ananielezea tunakokwenda!

**25: GRACE:** **(shouting)** Mbona anakwenda namna hiyo? Barabara yenyewe ina miinuko , hataweza kuona mashimo akiendelea namna hiyo kuzungumza naye.

**26. GRACE:** Dereva! Tahadhari, kuna gari linalokuja! Tahadhari! **(Shouting)** Gari laja mbele yako!

**27. SFX:** **Motorbike falling over and engine cutting out. Yelling by Peter and driver 2**

**<u>Scene Four – by the side of the road</u>**

**28. SFX Atmo:** **street traffic**

**29. GRACE:** Peter, uko salama?

**30. PETER:** Naam, Sijambo ila mguu wangu umekwaruzwa. Nimebahatika sijaanguka kwa kichwa lakini huyu dereva naona kama ameumia sana. Kichwa chake kimevimba. Nadhani amepoteza fahamu.

**31. GRACE:** **(speaking to driver 1)** Bora umepeleke mwenzako hospitalini. Amejeruhiwa kichwa. Tazama damu ilivyojaa kila mahali.

**32. DRIVER 1:** Mkosi gani huu! Sijui tutamwambia nini mwajiri wetu.

**33. GRACE:** Ati nini?! Lau mngekuwa mmevaa kofia za usalama, haya yasingewafika. Mpigie mwajiri wako simu sasa hivi ili huyu bwana apelekwe hospitalini la sivyo nitawapigia simu polisi.

**END OF SCENE FOUR**

**SHORT MUSIC**

**34. BEATRICE:** Naam, kama mlivyosikia katika kipindi cha saba cha mchezo wetu wa redio kuhusu usalama, watumizi wa pikipiki wana hatari zaidi ya kupata ajali na kwa hivyo ni muhimu kwao kuzingatia zaidi kanuni za usalama! Hapa studioni tunaye George, mtaalamu wetu wa usalama barabarani. Karibu George!

**35. GEORGE:** Asante.

**36. BEATRICE:** Eeeh, George, ni dhahiri kwamba Grace alikuwa na haki ya kuwa na wasiwasi kusafiria pikipiki bila kofia ya usalama.

**37. GEORGE:** Bila shaka na mwenye mwili ulinisisimka nilipokuwa nikikifuatilia kipindi hicho na kusikia kwmaba wote walikuwa wamepanda pikipiki bila kofia za usalama. Mwendesha pikipiki anapogingwa huwa kwenye hatari zaidi ya kupata majeraha. Tena mambo huwa mabaya zaidi ikiwa ataendesha pikipiki bila kofia ya usalama kwani huenda akapata majeraha ya kichwa ambayo ni hatari.

**38. BEATRICE:** Mbona watu wengi hawapendi kofia za usalama? Kofia zenyewe si ghali hivyo.

**39. GEORGE:** Inaelekea kana kwamba ni jambo la ada na pia, watu kutozingatia usalama wao au usalama wa abiria wao. Barani Afrika mara nyingi mimi hushuhudia waendesha pikipiki walio na hizo kofia lakini hawazivai inavyotakikana. Hivyo si vizuri na ni jambo la kuudhi sana hasa ukizingatia kuwa koia hiyo inaweza kukusalimisha na ajali mbaya.

**40. BEATRICE:** Vipi kuhusu hicho kipindi ambacho tumekisikiliza?

**41. GEORGE:** Naam, Peter na dereva wake walipata ajali ndogo, gari limegonga kioo cha upande mmoja pikipiki yao ikaanguka, hiyo si ajali kubwa lau ingekuwa inahusisha magari mawili. Lakini mtu anapoendesha pikipiki, ajali ndogo husababisha madhara makubwa. Dereva amejeruhiwa kichwa na amepoteza fahamu. Kama ingekuwa ajali kubwa angekuwa bila shaka amepoteza maisha.

**42. BEATRICE:** Inasikitisha sana. Ni kana kwamba dereva wa gari hakuwa akiziona pikipiki hizo mbili?

**43. GEORGE:** Ndiyo hivyo. Pikipiki zina umbo dogo sana hivi kwamba vigumu kwa madereva wa magari kuziona vizuri ziwapo barabarani. Sidhani kama madereva wote wawili walikuwa wamevaa mavazi yanayoangaza ya usalama. Mavazi hayo hung’aa gizani lakini pia hata na mchana mavazi hayo yanaweza kuokoa maisha. Mavazi hayo yanawatanabahisha madereva wa magari kwamba umo barabarani kwa hivyo hawawezi kukugonga. Ni jukumu lako kuhakikisha kwamba madereva wa magari mengine wanatambua kwamba upo barabarani.

**44. BEATRICE:** Ni jambo la kushtua kusikia abiria wanaotumia pikipiki hawana vifaa vya kujikinga endapo watakumbana na jambo fulani.

**45. GEORGE:** Unavyosema ni ukweli mtupu. Kuendesha pikipiki ni hatari sana na kwa hivyo hizi taratibu ndogo za kiusalama – kuvaa kofia na mavazi ya usalama - ni muhimu sana.

**46. BEATRICE:** Asante George.

**MUSIC (FADE UNDER OUTRO)**

**<u>OUTRO</u>**

**47. BEATRICE:** Katika kipindi kitakachofuata si siku ya kufurahisha kwa Alice na marafiki zake. Watakumbana na masaibu kwa kuendesha gari wakiwa walevi katika mchezo mwingine wa redio uliandikwa na Victoria Averill. Usikose kutusikiliza!

Ukitaka kusikiliza kipindi hiki kwa mara nyingine, basi tazama wavuti wetu www.dw.de/lbe. Asante sana kwa kujiunga nasi na jitahidi kuweka usalama barabarani!